MAMLAKA YA HALI YA HEWA
TANZANIA
# JARIDA LA HALI YA HEWA

**Na: 27. Msimu wa Kilimo 2018/19 Tathmini ya Kipindi cha Juni 11-20, 2019 na Matazamio kwa Kipindi cha Juni 21-30, 2019**

**Muhtasari**


- Hali ya ukavu inayotarajiwa itasaidia uvunaji,ukaushaji na utunzaji wa mazao .
- Maeneo mengi ya nchi yamepata vipindi vya hali ya ukavu kwa kipindi cha mwezi june 11-20, 2019.

## MIFUMO YA HALI YA HEWA KATIKA KIPINDI CHA JUNI 11-20, 2019

Katika siku kumi za dekadi, migandamizo mikubwa ya hewa iliyopo kaskazini mwa dunia (Azores na Siberia) iliendelea kudhoofika wakati ile iliyopo sehemu ya kusini mwa dunia (St. Helena na Mascarene) iliendelea kuimarika. Ukanda wa mvua ulielekea kaskazini zaidi ingawa sehemu yake ilikuwa ikigusa baadhi ya maeneo ya ukanda wa ziwa Victoria. Pamoja na kuimarika kwa mgandamizo mkubwa wa hewa ya kusini, kulikuwa na eneo lenye mgandamizo mdogo wa hewa katika kisiwa cha Madagasca hali iliyopelekea vipindi vya upepo mkali katika maeneo mengi ya nchi. Joto la bahari katika maeneo ya kusini magharibi mwa bahari ya Hindi lilikuwa la wastani na kusababisha kutokuwepo kwa vimbunga baharini. Upepo ulivuma kutoka kusini hadi kusini mashariki katika maeneo mengi ya nchi. Eneo la kusini mashariki mwa bahari ya Atlantiki (karibu na pwani ya Angola) lilikuwa na joto la bahari la wastani hadi juu kidogo ya wastani. Hali hii ilisababibisha kupunguza kwa mifumo ya kusababisha mvua katika maeneo ya magharibi mwa nchi.

## MWENENDO WA MVUA KATIKA KIPINDI CHA JUNI 11-20, 2019

Kwa kipindi hicho maeneo mengi ya nchi yalikua makavu isipokua kwa baadhi ya maeneo machache ya ukanda wa ziwa Viktoria na nyanda za juu kaskazini magharibi hususan mkoa wa mara na wilaya ya Ngorongoro ambayo yamepata mvua za nje ya msimu. Kiasi cha mvua kilichopimwa ni kati ya 26mm na 50mm kama inavyojionesha kenye kielelezo.




Kielelezo: Kiasi cha mvua katika kipindi cha Juni 11- 20, 2019

## TATHMINI YA HALI YA KILIMO KATIKA KIPINDI CHA JUNI 11-20, 2019

Katika kipindi cha dekadi iliyopita, kwa maeneo mengi yanayopata msimu mmoja wa mvua kwa mwaka hususan mikoa ya Mtwara, Tabora  na Kigoma shughuli za uvunaji wa mahindi zilikuwa zimekamilika ,wakulima waliendelea na shughuli za ukaushaji wa mahindi. Kwa mkoa wa Mbeya zao la mahindi limelipotiwa kuwa katika hatua ya kukomaa wakati huo Njombe, Iringa na Ruvuma wakulima waliendelea na uvunaji wa mahindi. zao la maharage limelipotiwa kuwa katika hali nzuri katika hatua ya kubeba kwa mkoa wa Mbeya ,kwa mkoa wa Tabora na Kigoma wakulima waliendelea  na shughuli za uvunaji wa mpunga na viazi. Kwa maeneo mengi yanayopata misimu miwili ya mvua kwa mwaka hususan mikoa ya Shinyanga, Mwanza, Tanga, Pwani na Manyara wakulima wamelijihusisha na uvunaji wa mpunga na viazi .kwa maeneo mengi yanayopata misimu miwili ya mvua kwa mwaka ,uvunaji wa mahindi umelipotiwa kwenye mikoa ya Shinyanga, Mara na Kagera. Kwa mkoa wa Kigoma , Mwanza na Shinyanga wakulima waliendelea na uvunaji wa zao la pamba .Maeneo mengi ya nchi yamendelea kupata upungufu wa

unyevuunyevu wa udongo. Upatikanaji wa malisho na maji ya mifugo nchini umeendelea kuwa wa wastani kwa maeneo mengi ya nchi isipokua Dodoma na Tabora amboka kumejitokeza vipindi vya upungufu wa mvua.

## HALI YA MAJI ILIVYOKUWA KATIKA KIPINDI CHA JUNI 11-20, 2019

Kina cha maji katika mabwawa na mitiririko wa maji kwenye mito vimeendelea kupungua kutoka na kuisha kwa msimu wa mvua .

## MIFUMO YA HALI YA HEWA INAVYOTARAJIWA KATIKA KIPINDI CHA JUNI 21-30, 2019

Katika kipindi hiki, migandamizo mikubwa ya hewa iliyopo kaskazini mwa dunia inatarajiwa kuendelea kudhoofika wakati ile iliyopo kusini inatarajiwa kuendelea kuimarika. Ukanda wa mvua unatarajiwa kuendelea kusogea kuelekea kaskazini hali itakayopelekea upepo kuvuma kutoka kusini hadi kusini mashariki katika maeneo mengi ya nchi ingawa sehemu yake inatarajiwa kuendelea kutawala mifumo ya hali ya hewa katika baadhi ya maeneo ya ukanda wa ziwa Victoria. Joto la bahari la wastani hadi chini ya wastani linatarajiwa katika eneo la kusinimagharibi mwa bahari ya Hindi hali itakayopunguza uwezekano wa kutokea vimbunga katika bahari. Upepo unatarajiwa kuvuma kutoka kusini hadi kusini mashariki hali itakayopekekea hali ya baridi katika maeneo mengi ya nchi. Eneo la Kusini mashariki mwa bahari ya Atlantiki (karibu na pwani ya Angola) kunatarajiwa kuwa na joto la bahari la wastani hadi juu kidogo ya wastani. Hali hii itapelekea kupunguza kwa upepo uvumao kutoka kagharibi hivyo kupunguza nguvu ya mifumo isababishayo mvua katika maeneo ya magharibi mwa nchi.

## HALI YA HEWA INAYOTARAJIWA KATIKA KIPINDI CHA JUNI 21-30, 2019

Maeneo ya Kanda ya ziwa Victoria (Mikoa ya Kagera, Geita, Shinyanga, Mwanza, Simiyu na Mara) yanatarajiwa kupata mvua zinazoambatana na ngurumo katika maeneo machache.

Maeneo ya pwani ya kaskazini (Mikoa ya Tanga, Maeneo ya kaskazini mwa Morogoro, Pwani na Dar es Salaam pamoja na visiwa vya Unguja na Pemba) yanatarajiwa kupata mvua nyepesi katika maeneo machache.

Maeneo ya Nyanda za juu kaskazini mashariki (Mikoa ya Arusha, Manyara na Kilimanjaro), magharibi mwa nchi (Mikoa ya Kigoma, Katavi na Tabora) na pwani ya kusini (Mikoa ya Mtwara na Lindi) yanatarajiwa kuwa Makavu kwa ujumla.

Kanda ya kati (Mikoa ya Dodoma na Singida), nyanda za juu kusini magharibi (Mikoa ya Rukwa, Songwe, Mbeya, Njombe na Iringa) na kanda ya kusini (Mkoa wa Ruvuma na Maeneo ya kusini mwa Morogoro) yanatarajiwa kuwa na hali ya Mawingu kiasi.

## MATARAJIO NA USHAURI KWA KILIMO KATIKA KIPINDI CHA JUNI 21-30,2019

Hali ya ukavu inayotarajiwa katika maeneo mengi ya nchi itasaidia shughuli za uvunaji, ukaushaji na uhifadhi wa mazao. Ingawaje hali hii ya ukavu itapelekea upungufu wa maji na malisho ya mifugo. Wafugaji wanashauriwa kutumia vizuri rasilimali za marisho na maji na kufuata ushauri unaotolewa na maafisa ugani.

## HALI YA MAJI INAVYOTARAJIWA KATIKA KIPINDI CHA JUNI 21-30, 2019.

Kina cha maji katika mabwawa na mtiririko wa maji kwenye mito vinatarajiwa kuendelea kupungua katika maeneo mengi nchini kutokana na kuisha kwa msimu wa mvua. Hata hivyo, wananchi wanashauriwa kutumia maji hayo kwa uangalifu hususan maeneo ambayo huwa yanakabiliwa na upungufu wa maji.

*Jarida limetayarishwa na:*

Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania
Ghorofa ya 3 -Ubungo Plaza – Barabara ya Morogoro, Dar es Salaam-Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

***S.L.P 3056; Simu. 255 -(0) 22 – 2460706-8; Nukushi: 255 - (0) 22 – 2460718 ; Barua pepe: (1) met@meteo.go.tz (2) agromet@meteo.go.tz; Tovuti: www.meteo.go.tz***